

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



TANGAZO

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI ANAPENDA KUVITANGAZIA VIKUNDI VYA **WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU** VILIVYO NA SIFA ZA KUPATA MIKOPO ISIYO NA RIBA KWA ROBO YA TATU NA YA NNE MWAKA WA FEDHA **2022/2023**, KUWA MANISPAA IMEANZA KUPOKEA MAOMBI YA MIKOPO HIYO ISIYO NA RIBA. KIASI CHA FEDHA KILICHOTENGWA KWA AJILI YA MIKOPO HIYO NI **4,685,514,600/-**, IKIWA NI **10% YA MAPATO YA NDANI YA MANISPAA**. HIVYO MNAOMBWA KULETA MAOMBI YA MIKOPO. MAOMBI HAYO YAANZIE NGAZI YA KATA, NA YAHAKIKIWE NA AFISA MAENDELEO YA JAMII NGAZI YA KATA, KISHA YAPITISHWE NA KAMATI YA MAENDELEO YA KATA.

MCHANGANUO WA FEDHA ZILIZOTENGWA KWA VIKUNDI HUSIKA NI KAMA IFUATAVYO:-

▪ VIKUNDI VYA WANAWAKE	-	1,873,005,840/-
▪ VIKUNDI VYA VIJANA	-	1,873,005,840/-
▪ VIKUNDI VYA WATU WENYE ULEMAVU	-	939,502,920/-

VICEZO

1. KIKUNDI KIWE KIMESAJILIWA
2. KIKUNDI KIWE NA KATIBA INAYOONESHA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA KIKUNDI
3. KIKUNDI KIWE NA MRADI / MIRADI NA SEHEMU MAALUM INAYOTAMBULIKA YA KUFANYIA SHUGHULI ZAO.
4. UMRI WA VIKUNDI VYA VIJANA NI KUANZIA MIAKA **18 – 35**
5. KIKUNDI LAZIMA KIWE NA AKAUNTI NAMBA YA BENKI KWA AJILI YA KUPITISHIWA MKOPO
6. IDADI YA WANACHAMA WA VIKUNDI VYA WANAWAKE NA VIJANA NI KUANZIA WATANO **(5)** NA KUENDELEA, WALEMAVU NI KUANZIA WAWILI **(2)**HADI WATANO **(5)**

VIAMBATANISHO:

1. NAKALA YA CHETI CHA USAJILI WA VIKUNDI
2. SLIP YA BENKI INAYOONYESHA AKAUNTI NAMBA YA KIKUNDI
3. MUHTASARI WA KIKAO CHA KIKUNDI WENYE AGENDA YA KUOMBA MKOPO
4. NAKALA YA LESENI YA BIASHARA
5. MCHANGANUO WA MRADI UONESHE GHARAMA ZA MRADI NA NAMNA UTAKAVYOREJESHA MKOPO HUO. (HIVI VYOTE VIWE KATIKA NAKALA TETE *softcopy*)

WOTE WENYE SIFA MNAKARIBISHWA

MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI HAYO NI TAREHE **30/04/2023** SAA **9:30** ALASIRI

Shedrack R. Maximilian

KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA